**BUKU LA 20**

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Heri za Mwaka Mpya Ninafuraha kuhusu kuweza kuanza mpya wa 2021. Asante kwa washikadau wetu wote wa jamii kwa uthabiti wenu, bidii, uvumilivu, na ujasiri katika mwaka wa 2020. Ninatazamia kuwa na fursa ya kukamilisha mwaka huu wa masomo nikiwa imara licha ya nyakati hizi zisizo na kifani.

Ningependa kuwashukuru wafanyakazi wetu ambao wamewajibika kufanya mambo ambayo hayajawahi kufanywa awali katika historia ya masomo, na kwa hiyo wilaya inashukuru. Nilifurahi kuona waalimu wengi sana ambao waliweza kurudi huku wakiwa nje wakizuru shule wiki hii. Wengi walitoa ahadi yao kwa wanafunzi wetu na wamefurahi kuhusu kurudi kwa majengo ya shule. Wakati wa ziara zangu, nilikuwa na fursa ya kukagua ishara za usalama, vituo vya kunawa mikono, na mikutano ya mtandaoni ya wafanyakazi. Tunapoendelea mbele na masomo mseto, tafadhali fahamu kwamba ninasikiliza hoja zenu. Sitaki kupuuza changamoto zilizopo, lakini ninahisi ninahimizwa na juhudi zenu.

**<u>Utayarishaji wa Majengo</u>**

Mazingira salama na mazuri ya masomo ya ana kwa ana ndio kipaumbele chetu cha juu. Timu ya Operations inatumia viwango vya utayarishaji wa majengo kuhakikisha kila kituo na shule kiko tayari kuwakaribisha wafanyakazi na wanafunzi katika mazingira salama ya kusoma. Utayarishaji wa shule wa DCSD unajumuisha kaguzi muhimu zifuatazo:

- Bidhaa za Kujikinga (PPE) na Bidhaa za Usafi
- Usambazaji wa Bidhaa za Usafi na Taratibu
- Kukaa Mbali na Wengine na Kupanga Nafasi
- Kupata Maji
- Mabomba na Mifumo ya HVAC
- Ishara za Usalama za COVID-19 shuleni

Huku DCSD ikiwa tayari kufungua shule tena, vituo vya DCSD vimejiandaa kwa kiwango cha asilimia 75%. Utayarishaji wa majengo ni mchakato unaoendelea na

uongozi wa Wilaya utaendelea kujenga njia za kutembelea na kufuatilia njia mpya na itifaki za usalama baada ya wanafunzi na wafanyakazi kurudi katika masomo ya ana kwa ana.

Kama ilivyosemwa mwaka mpya, sayansi imebadilika kulingana na mwongozo uliosasishwa kutoka kwa CDC ikiwemo viwango vya visa na uwezo wa shule kutekeleza mikakati tano muhimu ya kupunguza hatari ya maambukizi ya COVID-19 shuleni. Kutekeleza mikakati hii itakuwa muhimu katika kuhakikisha wafanyakazi na wanafunzi wetu wako salama wakati wa janga hili.

**Mikakati ya Kupunguza Hatari**

Mikakati tano muhimu ya CDS ya kupunguza zaidi hatari ya maambukizi na maenezi ya COVID-19 shuleni ni:

- Matumizi sahihi na ya mara kwa mara ya barakoa
- Kutokaribiana na watu ikiwa inawezekana
- Kunawa mikono
- Kusafisha na kuua vidudu
- Kuwafuatilia watu waliokaribiana kwa kushirikiana na Bodi ya Afya ya DeKalb

Tunawahimiza wanafunzi kuzoea mikakati hii mipya sasa, ili wakati wanapoanza kurudi shuleni, kuvaa barakoa, kutokaribiana na wengine, na kunawa mikono kuwe mambo ya kawaida.

Ijapokuwa kunawa mikono ni njia muhimu ya kukomesha kuenea kwa vijidudu na kupunguza hatari ya kueneza virusi vya COVID-19, kunawa mikono kwa maji na sabuni kwa angalau sekunde 20 au kutumia kieuzi cha mikono kilichotengenezwa kwa pombe kilicho na angalau asilimia 60 ya pombe ikiwa sabuni na maji hazipatiani – hupunguza kuenea kwa vijidudu ambavyo vinaweza kusababisha ugonjwa, kulingana na CDC.  Maji moto na baridi huondoa viwango sawa vya wadudu kutoka kwa mikono yako.

Itifaki zote za usalama zinalingana na mwongozo wa afya uliotolewa na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) na Bodi ya Afya ya Kaunti ya DeKalb ili kupunguza kuenea kwa COVID-19.  Kwa maelezo zaidi kuhusu kunawa mikono

vizuri, tafadhali tembelea tovuti ya CDC, na kwa mwongozo husika wa Operations COVID-19, tafadhali tembelea https://www.dekalbschoolsga.org/school-reopening/safety-protocol/.

**Wafanyakazi na Kazi Mbadala**

Tunaelewa kwamba wafanyakazi wanafanya wawezavyo kwa ajili ya familia zao na maslahi yao ni muhimu katika kuunga mkono wanafunzi na wilaya yetu. Baadhi ya wafanyakazi wetu wamewasilisha ombi la ugumu, ambayo ni mbinu ya kuwasilisha hoja au tatizo unaloweza kuwa nalo la kurudi katika majengo au ratiba ya kazi yako. Wafanyakazi wote wanaweza kuomba ombi la ugumu. Hata hivyo, huenda kazi mbadala (AWA) isiwe sawa kwa wafanyakazi wote. AWA inategemea majukumu msingi ya wafanyakazi. Ikiwa kazi ya wafanyakazi inawahitaji kukutana ana kwa ana, basi muda wa kufanya kazi kwa mbali utaongezwa. Chaguo tofauti linapaswa kuzingatiwa, kama vile Ratiba Iliyorekebishwa ya Kazi au Eneo/Mahali Mbadala pa Kazi.

Wafanyakazi wanaostahiki wanaweza kustahiki na kuomba malazi chini ya Sheria ya Wamerikani walio na Ulemavu (ADA). Wafanyakazi, wanaoamini wana hali ya kimatibabu ambayo inawafanya wahitimu malazi ya ADA, lazima wakamilishe maombi ya ADA na kutoa cheti cha matibabu ili kuanza mchakato huu. Rasilimali Watu wamejitolea kujibu mchakato huu wote wa maombi na, yakiidhinishwa, kuunda mpango unaofaa.

Ikiwa una wasiwasi au maswali yoyote, tafadhali yashiriki na msimamizi wako wa sasa. Ikiwa huwezi kurudi mara moja, ninajua ilikuwa uamuzi mgumu. Tafadhali kuwa na uhakika kwamba ikiwa uliwasilisha ombi la muda la ugumu, hoja zako zimepitiwa na kuzingatiwa na Wilaya. Maombi Yote ya Ugumu yatapitiwa na kutekelezwa kwa kipindi cha siku 30 hadi Februari 2, 2021. Fomu zinapatikana kwenye Kituo cha Wafanyakazi chini ya ukurasa wa Divisheni ya Rasilimali Watu. Tena, asante kwa kazi yako ngumu na uvumilivu tunapokuwa tukipitia nyakati hizi zisizo na kifani.

**Familia za DCSD**

Huku familia zetu zikiamua kama kurudi shuleni ndio chaguo sahihi kwao, tafadhali endelea kutembelea tovuti yetu ya kufungua shule tena kwa maelezo muhimu kuhusu

masomo ya mtandaoni, usafiri, itifaki za usalama, na zaidi. Ninahimiza pia familia zetu kutazama mkutano wetu wa Bodi mnamo tarehe 11 Januari, 2021, saa 11:30 am kwa Mkutano wa Mtandaoni wa Mchango wa Jamii.  Tutatoa taarifa muhimu kuhusu masomo ya ana kwa ana. Unaweza kutazama mkutano huu kwenye kituo 24 katika Kaunti ya DeKalb au kwenye DSTV online.

Mnamo Jumamosi, Januari 9, tunasheherekea Siku ya Maafisa wa Shule. Tungependa kuwashukuru Maafisa wetu wa Shule kwa kujitolea kwao kwa usalama wa wanafunzi, wafanyakazi, familia na jamii yetu.

Mwishowe, wengi wa wanafunzi, wafanyakazi, na familia zetu walishuhudia mzozo wa umma wiki hii wakati Makao yetu Makuu ya kitaifa yaliposhambuliwa. Picha hizi zilikuwa za kusumbua na za kutisha kwa wanafunzi wetu wachanga. Tuchukue muda huu kusikiliza na kuanzisha mazungumzo mema na ya kujali kuhusu utofauti wa kimaoni. Baada ya kupitia mwaka wa 2020 uliokuwa na changamoto, wanafunzi wetu wanahitaji msaada wetu na nafasi salama ya kushiriki wasiwasi na mawazo yao.

Ninatazamia mwaka mwema wa 2021 na ninahimiza jamii yetu thabiti kuendelea mbele na juu!

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris